

Fever in Children (Swahili)

Homa kwa watoto



Mtoto ana homa ikiwa joto lake ni kubwa kuliko 38°C. Watoto wote watakuwa na homa wakati fulani. Ni moja ya sababu za kawaida kwa watoto kumwona daktari na mara nyingi husababisha wazazi kuhangaika. Hata hivyo, ni adimu sana kwa homa kusababisha madhara ya muda mrefu.



Homa ni alama kuwa mfumo wa kinga wa mtoto wako hupambana na maambukizi. Homa haitamdhuru mtoto wako, lakini inaweza kusababisha mshtuko wa homa (au kifafa cha homa au kifafa) katika karibu 1 wa watoto 30.

Homa nyingi kwa watoto husababishwa na maambukizi ya virusi. Kulingana na dalili zingine za mtoto wako, daktari wako anaweza kufanya vipimo kadhaa ili kubaini bakteria au virusi vinavyosababisha homa. Kumbuka, homa haisababishwi na meno.

Utunzaji wa nyumbani

Ikiwa mtoto wako ana homa, unaweza kumsaidia kujisikia vizuri kwa:

- kuhakikisha anakunywa maji mengi ya kisukari
- kumvisha nguo nyepesi na za starehe
- kumpa paracetamol ya watoto (Panadol, Dymadon) au ibuprofen (Nurofen). Fuata maelekezo ya chupa au paketi kwa kipimo sahihi. Usimpe zaidi kuliko kiasi kilichopendekezwa ndani ya saa 24.
- kuepuka sifongo na bafu za baridi.

Kwa ushauri wa matibabu usio wa dharura, piga simu 13 HEALTH (13 43 25 84) kuzungumza na muuguzi aliyesajiliwa saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki kwa gharama ya simu ya mtaa.



omba kupata mkalimani ikiwa unamhitaji.

Jinsi ya kupima joto la mtoto wako

Unaweza kupima joto la mtoto wako kwa:

- kuweka kipimajoto chini ya kwapa kwake
- kuweka kwa upole kipimajoto katika sikio lake (ikiwa mtoto wako ana miezi 6 au zaidi).


Vihisi vya infrared na vibandiko vya kubandika **havitapima** kwa usahihi halijoto ya mtoto wako.



Wakati wa kumona daktari

Mpeleke mtoto wako kwa idara ya dharura ya hospitali iliyo karibu nawe ikiwa halijoto yao ni **juu zaidi ya 38°C** na yeye:

- ana umri chini ya miezi 3
- anaonekana mgonjwa sana au kuduwaa
- ni mgumu kuamka
- analia sana na ni mgumu wa kutuliza
- anakunywa au kukojoa kidogo kuliko kawaida
- ana tatizo ya kumeza au kumwaga mate
- amekosa nguvu au hatumii mikono na miguu yake.
- anajitahidi kupumua
- ana maumivu makali ya tumbo
- ana shingo ngumu na ni nyeti kwa mwanga
- ana ngozi ya bluu, rangi ya kijivu, yenye madoadoa, au madoa ya rangi ya zambarau
- ana unyeundu au uvimbe kwa mwili wake.
- anasikia maumivu anapokojoa



Piga simu kwenye Sifuri Mara Tatu (000) mara moja ikiwa mtoto wako akijitahidi kupumua, midomo yake inakuwa bluu, au anapata kifafa.

Imeandaliwa na Idara ya Dharura, Hospitali ya Watoto ya Queensland. Tunatambua mchango wa watumiaji na walezi. **ID ya Resource ID: FS013 Reviewed: July 2022**

Kanusho: Maeleo haya yametolewa na wataalamu wa afya kama mwongozo pekee na yanalenga kusaidia, si kubadili nafasi, majadiliano na daktari wa mtoto wako au wataalamu wa afya. Taarifa husashishwa kila mara, kwa hivyo tafadhalii angalia kuwa unarejelea toleo la hivi majuzi zaidi. Tafuta ushauri wa matibabu, inapofaa, kwa wasiwasi kuhusu afya ya mtoto wako.